# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

SHULE YA SEKONDARI NAMAYUNI,
S.L.P 04,
**KILWA – MASOKO.**
TAREHE 15/12/2029

**NDUGU**
…………………………………………………......
……………………………………………………..

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA SHULE YA SEKONDARI NAMAYUNI</u>**

Rejea mada ya hapo juu.
Nakujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari katika Shule ya Sekondari NAMAYUNI, Shule ipo katika Kata ya NAMAYUNI Wilaya ya KILWA.
Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020 saa 01:00 Asubuhi. Unatakiwa kuripoti siku hiyo kwa ajili ya Usajili na kuanza masomo rasmi.

1. **AFYA**
   Kabla ya kuripoti Shuleni unatakiwa ukapime Afya yako na Mganga wa Kituo cha Afya Au Hospitali ya Serikali na sio katika Zahanati ambazo hazina Maabara za vipimo (Angalia nyuma ya barua hii)

2. **SARE ZA SHULE**
   **(a) WAVULANA:**
   - (i) Suruali mbili (2), Nyekundu (1) na Khaki (1).
   - (ii) Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi (Tomato).
   - (iii) Viatu vyeusi Jozi mbili (2).
   - (iv) Soksi nyeupe jozi mbili (2).
   - (v) Raba za Michezo na bukta na t shirt rangi ya kijani
   - (vi) Begi dogo la kubebea Madftari (Sio vifungashio).

   ***NB:*** Ni marufuku kuvaa Suruali ya Shule bila Mkanda au bila kuchomekea shati. Aidha ni marufuku kuvaa suruali nyembamba (MODO).

   **(b) WASICHANA:**
   - (i) Sketi mbili (2), Nyekundu (1) na Khaki (1).
   - (ii) Mashati mawili (2) meupe nusu kanz.
   - (iii) Viatu vyeusi Jozi mbili (2).
   - (iv) Soksi nyeupe jozi mbili (2).
   - (v) Wasichana wanaruhusiwa kuvaa **HIJABU** nyeupe na isiwe na mapambo.(urembo)iwe ya kushona.
   - (vi) HIJABU iwe duara na ifunike mikono na sketi iwe ndefu.(sketi fupi haziruhusiwi)
   - (vii) Raba za Michezo na sare za michezo t shirt na tracksuit ya bluu.
   - (viii) Begi dogo la kubebea Madftari (Sio vifungashio.)

3. **VIFAA VINGINE (MAAGIZO)**
   **(a) WAVULANA:**
   - (i) Jembe lenye mpini imara.

(ii) Kisado (Ndoo ya Plastiki ndogo moja na fagio la chelewa la wima moja).

**(b) WASICHANA:**

(i) Fyekeo(Kwanja moja).

(ii) Kisado (Ndoo ya Plastiki ndogo moja na fagio la chelewa la wima moja)

**4. PICHA ZA PASSPORT SIZE MBILI(2)**

**5. MAHITAJI BINAFSI YA KITAALUMA**

(a) Daftari kubwa za kutosha Masomo (10) aina ya Kaunta buku ziwe (10).

(b) Daftari ndogo za majaribio kumi.(10)

(c) Mathematical set (Compass)au mkebe.

(d) File moja ya kuhifadhia mitihani

(e) Rula

(f) Peni na penseli.

(g) Mchango wa chakula 9000/= utakaopokelewa na kamati ya wazazi.(ukifika shule utaelekezwa)

**6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:**

(a) Heshima kwa Viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na Ratiba ya Shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)ili kuboresha taaluma ya mwanafunzi.

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa Uanafunzi wako katika Shule hii.

(f) Kutunza usafi wa Mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

(i) Kutunza mali za umma.

***7. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule***

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana Au kupiga.

(f) Kuharibu kwa maksudi mali ya umma.

(g) Kudharau Bendera ya Taifa.

(h) Kuwa Mjamzito / kupata mimba.

(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kutoa mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au Watu.

(l) Kukataa adhabu kwa maksudi.

(m) Kuwa na simu ya mkononi.

***8. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi:***

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti Shuleni.

(b) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

***NB:***

(a) Kumbuka Shule hii ni ya kutwa mahitaji mengine akamilishiwe mtoto na mzazi au mlezi anayeishi nae. Mahitaji hayo ni kama suala la afya, malazi, chakula, ulinzi na usalama wa mtoto pia kumbuka kutokumleta mtoto ni kosa kisheria na unaweza kuchukuliwa hatua.
(b) Pia mzazi/mlezi unatakiwa kumleta Mwanafunzi (kijana wako) akiwa amevaa sare halisi za Shule, viatu na soksi zinazotakiwa na pia uwe umekamilisha mahitaji na taratibu zote kama ulivyoelekezwa katika barua hii.

**KARIBU NAMAYUNI SEKONDARI**

KAPINGA.A.J.

MKUU WA SHULE.

## UTHIBITISHO/KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi …………………………………………………………………………………………. Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………….. Kidato cha …………………………… Mwaka ………………………….. nakubali asome katika Shule ya Sekondari ya Kutwa Namayuni. Nitahakikisha Mwanafunzi huyu anaendelea vizuri kimasomo hivyo:-

(a) Hana ruhusa ya kwenda kwenye nyumba za Wageni, maeneo ya ulevi, ,maeneo ya michezo ya kamari,kumbi za starehe au Taarabau n.k.
(b) Mimi Mzazi/Mlezi nitampatia vifaa vyote vinavyohitajika hapa Shuleni kama vilivyoainishwa.
(c) Ninaahidi kuwa nitahakikisha mtoto anafuata sheria na taratibu za Shule, hatua kali ichukuliwe dhidi yake kama atavunja taratibu na sheria za Shule.
(d) Ninaahidi kumleta Shuleni mtoto wangu kwa wakati uliopangwa na Uongozi wa Shule bila kuchelewa.
(e) Anwani yangu ni:
……………………………………………
……………………………………………

Kazi ya Mzazi/Mlezi: Baba ………………………………………..
Mama ……………………………………..
Namba ya simu: Baba ………………………………………..
Mama ……………………………………..
Saini ya Mzazi/Mlezi: ………………………………….. Tarehe ………………………..
Jina la Mwanafunzi: …………………………………….
Saini ya Mwanafunzi …………………………………….. Tarehe ………………………

NAMAYUNI SECONDARI
DISPLINE,HARD WORKING AND EXCELLENCE PERFORMANCE.

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

# NAMAYUNI SEKONDARY SCHOOL

P.O. BOX 04
**KILWA MASOKO.**
DATE ……/…./…….

***To the Medical Officer,***
…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
Name of Student: Mr/Miss ……………………………………………………………………………………………
Form ………………………………………………… Term …………………... Year ………………………………………...

***Dear Doctor,***

I shall very grateful if you kindly examine the above named Student and send us a report regarding his/her health condition for his/her suitability in undertaking studies.

| | | |
|---|---|---|
| 1. X – Ray ( ) | 2. Urine ( ) | 3. Stool ( ) |
| 4. V.D ( ) | 5. Tuberculosis ( ) | 6. Physical fitness ( ) |
| 7. Pregnancy ( ) | | |

**A. PRELIMINARY INFORMATION (BY STUDENT BEFORE THE DOCTOR)**

| No | DISEASES | YES | NO | No | | YES | NO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1<br>2<br>3<br>4<br>5<br>6<br>7<br>8<br>9<br>10 | Tuberculosis<br>Pneumonia<br>Asthma<br>Heart trouble<br>Recurrent Indigestion<br>Jaundice<br>Dysentery<br>Kidney and urinary<br>trouble<br>Nervous Breakdown<br>Diabetes | | | 11<br>12<br>13<br>14<br>15<br>16<br>17<br>18<br>19 | Epilepsy<br>Ear, nose and Throat<br>troubles<br>Skin disorder disease<br>Anemia<br>Operations<br>Serious accident<br>Malaria<br>Stomach trouble<br>Eye disorder | | |

**B. OFFICIAL MEDICAL EXAMINATION REPORT**

(a) Weight
(b) Heart Beat
(c) Vision e.t.c

……………………….....
**KAPINGA.A.J.**

**HEADMASTER.**
**NAMAYUNI SECONDARY.**